



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

## TAARIFA KWA UMMA

---

### **KUHUSU MAOMBI YA KAZI ZA MUDA ZA SENSA YA WATU NA MAKAZI YA MWAKA 2022, TAREHE 27 MEI 2022 OFISI YA TAIFA YA TAKWIMU - DODOMA**

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Tarehe 05 Mei, 2022, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitangaza rasmi kuanza kupokea maombi ya kazi za muda za makarani na wasimamizi wa Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika tarehe 23 Agosti, 2022 kupitia Mfumo wa Maombi wa Kielektoniki. Muda wa maombi hayo ulifikia tamati tarehe 19 Mei, 2022 ambapo idadi ya waombaji ilifikia 689,935 kati ya 205,000 wanaohitajika kwenye zoezi la Sensa ya Watu na Makazi.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Leo tumekutana hapa ili kutoa taarifa kwa umma kuhusu taarifa zisizo rasmi zinazosambaa mitandaoni kuhusu orodha ya majina ya makarani yenye kichwa cha habari "ORODHA YA MAJINA YA MAOMBI YA KAZI YA MUDA YA SENSA YA WATU NA MAKAZI YALIYOHAKIKIWA NA KUJIBIWA KIKAMILIFU".

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Taarifa hii sio rasmi kwa Watanzania waliomba nafasi za Ukarani na Usimamizi wa Sensa katika maeneo wanayoishi. Aidha, kwenye taarifa inayofanana na hii ambayo pia sio rasmi, watu hawa ambao hawana nia nzuri kwa Serikali na watanzania kwa ujumla wamekwenda mbali na kutamka tarehe ya usaili kuwa ni **29 Mei 2022.**

Napenda ifahamike kwamba, mchakato wa ajira za muda za makarani na wasimamizi wa Sensa bado unaendelea katika ngazi ya Kata/Shehia na Halmashauri zote. Zoezi la uchambuzi wa maombi kwa waombaji wote linatarajiwa kuanza tarehe **02 Juni 2022** kwenye kila Kata au Shehia husika baada ya kukamilika kwa mafunzo ya maafisa wataohusika kufanya usaili. Mchakato wa ajira za Makarani na Wasimamizi wa Sensa linakwenda vizuri kulingana na ratiba ya Sensa.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Naomba mfikishe ujumbe huu kwa Watanzania wote kwamba taarifa yoyote kuhusu mwenendo wa maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi, Sensa ya Majengo na Sensa ya Anwani za Makazi ikiwemo ajira hizi za muda itatolewa na Serikali kupitia vyombo vya habari

**Ahsanteni kwa Kunisikiliza**



**Jiandae Kuhesabiwa Siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022**